



Mkuu wa Mawasiliano wa Kampuni ya Saruji Tanga, Kati Kerenge (katikati), akionyesha tuzo mbili za NBAA ambazo kampuni yao imeshinda wakati wa mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Jayne Nyimbo na kulia ni Mhasibu wa Tanga Cement, Edgar Mlenge.

Mbunge: Askari achapwe viboko

Na Nakajumo James, Moshi

MBUNGE wa Vunjo, Aloyce Kimaro, ametoa agizo la kukamatwa mlinzi wa Hospitali ya Kilema na kuchapwa viboko hadharani kwa madai ya kutishia maisha na kumdhaliisha Mganga Mkuu wa hospitali hiyo.

Kimaro aliagiza serikali ya kijiji cha Mshashi Kilema, Moshi Vijijini kutekeleza agizo hilo mara moja na kukomesha tabia ya mlinzi huyo.

Kauli hiyo ilitokana na malalamiko ya Mganga Mkuu, Sista Clarista Massawe, kwamba mlinzi Samwel Shayo alitishia kumuua na kumtukana matusi ya nguoni na kumfanyia vurugu.

TCCL: Bidhaa, kazi zetu ni bora

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Saruji ya Tanga (TCCL) imeibuka mshindi wa tuzo bora ya hesabu za mashirika kwa mwaka 2008.

Tuzo hizo zilizoandaliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) zilitolewa hivi

karibuni katika sherehe zilizo-fanyika mjini Arusha.

Akizunguma na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCCL, Jayne Nyimbo alisema tuzo hiyo ni ishara kuwa kampuni hiyo inafanya kazi kwa kuzingatia ubora.

"Ni mafanikio makubwa kwetu kwamba kampuni yetu imepiga

hatua kubwa na kukidhi viwango vya hesabu za kihesabu za kimataifa," alisema.

Aliongeza: "Mafanikio hayo yanaiweka vizuri sura ya kampuni kwa wawekezaji na wana hisa."

Nyimbo alisema kilichosababisha mafanikio hayo ni kufanya kazi kwa uwazi na kujitolea na ni matokeo ya kuwa na timu bora ya uongozi na wafanyakazi.